kwenye ulimwengu mzima

15. Ruth Mbennah, mratibu wa Project Hannah wa Afrika Kusini na Mashariki anapowatia moyo, kuwapenda na kuwafundisha wanawake ili kumtumikia Mungu pamoja na wenzao vizuri zaidi. Ombea afya ya Ruth na usalama wake anaposafiri kukutana na timu zingine.
16. Brenda Lombard anapowatia moyo na kusaidia timu za Afrika za kitaifa kuandaa taarifa zinazohitajika kila mwezi na kalenda za maombi za kila mwezi kwa lugha zaidi ya 10.
17. Nguvu na hekima kwa Esperança, ambaye ameongoza huduma ya Project Hannah nchini Msumbiji tangu mwaka 2005. Ombea timu ya waandaaji wa kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* kwa kireno (Esperança, Constância, naTahera) na wanaoandaa kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* kwa lugha ya Makhuwa (Maria na Delcia). Omba ili vipindi vya *Wanawake wa Matumaini* viandaliwe kwa lugha nyingi zaidi. Kireno hufundiswa mashuleni lakini wanawake wengi hawapati fursa ya kwenda shule.
18. Viongozi wa kanisa na jamii wawe majasiri na wafundishwe umuhimu wa kuwaheshimu watu wote kama watoto wa thamani wa Mungu. Omba ili familia ziwe mfano wa heshima kwa wanawake na wasichana ili vurugu majumbani zisivumiliwe.
19. Amani na usalama kaskazini mwa Msumbiji.Ombea wananchi wa kawaida 11,500 ambao wamehama Msumbiji tangu shughuli za kijeshi zilipoanza Oktoba 2015 za kuwanyang'anya waasi silaha kwenye eneo la mpakani mwa Malawi.
20. Wazazi na walio na mamlaka wafanye kila jitihada kutokomeza utamaduni wa ndoa za utotoni na kuwapa watoto wa kike elimu inayofaa. Kwenye baadhi ya maeneo nchini Msumbiji, asilimia 68 ya wanawake huolewa wakiwa na umri chini ya miaka 18 na wengine wengi kabla ya kufikisha miaka 15. Ombea viongozi wa jamii waunge mkono mpango mpya wa kitaifa wa kutokomeza ndoa za utotoni na kusaidia kubadilisha tabia za wasichana.
21. Wanawake wakristo ambao bado ni vijana kuelewa umuhimu wa kuolewa na waamini na kuwalea watoto wao katika njia ya kumfuata Kristo.
22. Wanawake nchini Msumbiji ambako chini ya mtu mmoja kati ya wanne hapati huduma za kisasa za usafi na karibia nusu ya watu wote wanakunywa maji kutoka kwenye vyanzo ambavyo si salama.
23. Waombaji wa Project Hannah nchini Msumbiji na zaidi ya watu 1,000 kwenye vikundi vya maombi wahisi upendo wa Mungu na uwezo wake kwenye nyumba zao na kwenye jamii.
24. Wanawake wanaojaribu kuzihudumia familia zao. Pamoja na ukuaji wa uchumi wa hivi karibuni, zaidi ya nusu ya watu milioni 24 nchini Msumbiji wanaendelea kuishi chini ya kiwango cha umaskini.
25. Familia za wanawake waliofariki wakati wa kujifungua wakiwa nje ya vituo vya afya au kwa kuhudumiwa na watu wasiokuwa na ujuzi. Baadhi ya taratibu za kimila hufanya akina mama wasipate huduma zinazohitajika. Wanawake chini ya nusu (asilimia 44) ya wanaojifungua ndio wanaopata huduma ya wataalamu.
26. Wanawake wenye ndugu ambao ni walevi au watumiaji wa madawa ya kulevya.
27. Wasichana waliolazimishwa kuingia kwenye ndoa na wapo hatarini kupata maambukizi ya VVU. Baadhi ya wasichana walioolewa asilimia 19 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19 wapo kwenye ndoa zenye mke zaidi ya mmoja. VVU vinatokea mara tatu zaidi kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15 na 24 kuliko wavulana wenye umri huo.
28. Mvua nchini Angola na Msumbiji ziwe za mara kwa mara na za kiasi ili mazao yakue na watu waondokane na ukosefu wa chakula na umaskini wa kutisha wanaoteseka nao.
29. Viongozi wa kanisa nchini Angola ma Msumbiji waelewe kuwa Project Hannah sio dhehebu bali ni huduma ya kusaidia mikusanyiko ya wanawake kuwa mama, wake, dada mabinti na bibi wanaomcha Mungu.
30. Wanawake wanaotumia matangazo ya *Wanawake wa Matumaini* yanayorushwa na redio kama fursa ya kuwaalika marafiki na familia kuweza kusikiliza vipindi pamoja na kujadiliana mambo ya maandiko pamoja . Omba ili wamjue Mungu: *"Niombeeni neno la Bwana liendelee, na kutukuzwa vilevile kama ilivyo kwenu."* (2 Wathesalonike 3:1).

| **Usikose kusikiliza kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* kwa siku na saa kama ifuatavyo:** | |
|---|---|
| • Kwa wakazi wa Moshi - Radio sauti ya Injili 96.2 FM : Siku ya Jumapili Saa 12:00 hadi saa 12:30 jioni. | • Kwa wakazi wa Dar es Salaam - Radio Wapo 98.1 FM: Siku ya Jumapili saa 9:30 hadi saa 10:00 mchana. |
| • Kwa wakazi wa Mwanza - Neema Radio – 98.2 FM : Siku ya Jumanne saa 2:00 Hadi saa 2:30 Usiku. | • Kwa wakazi wa Arusha - Radio safina 92.6 FM: Siku ya Jumapili saa 1:30 hadi saa 2:00 Usiku. |
| • Kwa wakazi wa Dodoma – Radio Uzima 94.0 FM Siku ya Jumatatu na Ijumaa Saa 2:30 hadi saa 3:00 Usiku. | • Kwa wakazi wa Zanzibar- Zenj Radio – 96.9 FM : Siku ya Jumanne saa 3:00 hadi saa 3:30 Usiku. |

**Kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* kinarushwa kwa zaidi ya lugha 65.**
**Kalenda maombi ya PH ya kila mwezi hutafsiriwa kwa zaidi ya lugha 85.**

# KUWAOMBEA *Wanawake* WA ANGOLA NA MSUMBIJI



PROJECT HANNAH
PRAYER CALENDAR
***JUNE 2016***
***Swahili***

Project Hannah

Huduma ya maombi ya Project Hannah nchini Angola ilianza mwaka 2001. Vikundi vya maombi vikakua upesi na maisha ya wanawake yakabadilika walipomuona Mungu akitenda kazi kwenye nyumba zao, jamii na makanisa. Mwaka 2005, wanawake wa Msumbiji nao pia walianzisha vikundi vya maombi nao pia wakamuona Mungu a akitenda miujiza kwenye maisha yao. Wanawake hawa wanakutana na changamoto nyingi (umaskini mkubwa, tiba ya afya hafifu, kukosa elimu, ndoa za utitoni, ulevi na madawa ya kulevya, ukame na mafuriko na matatizo makubwa ya usafi). Hata hivyo wanajua kuwa Mungu anasikia maombi yao na kwamba kuna nguvu ya kutembea naye kwenye mazingira ya kutisha ya kukosa haki wanayoishi nayo kila siku.

Almasi na mafuta yameifanya Angola kuwa nchi ya tatu kiuchumi kusini mwa jangwa la Sahara. Hata hivyo, inakadiriwa kuwa asilimia 70 ya wakazi wake wanaishi kwa kiwango cha chini ya doka 2 kwa siku. Mji mkuu Luand unachukuliwa kuwa wa gharama sana ulimwenguni kwa wakazi wageni ; hata hivyo zaidi ya asilimia 70 wanaishi kwenye vibanda. Vifo vya watoto wachanga ni kubwa ulimwenguni. Mtoto mmoja hufa kabla ya kufikisha miaka mitano, idadi ya pili kwa ukubwa ulimwenguni. Wanawake chini ya asilimia 54 ndio wanaoweza kusoma.

Upatikanaji gesi kwenye pwani ya Msumbiji mwaka 2011 umeleta mabadiliko kidogo sana kubadili uchumi wa moja ya nchi maskini ulimwenguni. Zaidi ya nusu ya watu milioni 24 wanaishi chini ya kiwango cha umaskini. Takriban nusu ya watu hawapati maji safi na salama. Msumbiji ni nchi ya saba duniani kwa ndoa za watoto ulimwenguni.

Mafuriko kaskazini mwa Msumbiji mwaka huu yameathiri zaidi ya watu 32,000 na kuharibu nyumba 4,991 na madarasa 303. Wakati huo huo, Msumbiji kusini kuna kiangazi cha kutisha katika miaka 35. Takriban watu milioni 1.5 wanateseka kwa kukosa chakula. Maeneo ya kilimo kusini mwa Angola pia yanateseka kwa kiasi cha kutisha.

## Tafadhali omba kwa ajili ya...

1. Wanawake wa Angola na Msumbiji wanapokabiliana na magumu ya maisha ya kila siku na maumivu na makovu ya kunyanyasika. Omba ili wapate amani na matumaini kwa Bwana Yesu Kristo *(Warumi 15:13)*.
2. Viongozi wa vikundi vya maombi vya Project Hannah, waombaji na watu wanaojitolea nchini Angola na Msumbiji wanapofundisha masomo ya Biblia, kutembelea wagonjwa na walio wapweke, kufanya uinjilisti, kuwatia moyo na kuwafariji kwa njia ya urafiki na maombi.
3. Timu ya Project Hannah nchini Angola: Marcolina, Josefina, Juliana, na Justina. Ombea maandalizi ya kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* cha Umbundu kiweze kurejea kurushwa hivi karibuni. Waombee wasikilizaji wa kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* cha kireno.
4. Waombaji 2,581 wa Angola na vikundi 153 vya maombi kuwa na umoja ndani ya Kristo na kushiriki kwenye furaha ya kumtumikia pamoja kwa upendo na unyenyekevu.
5. Huduma nzuri ya afya kwa watu wa Angola wanaoishi kwenye ukanda wenye homa ya njano barani Afrika ambapo asilimia 90 ya watu 60,000 hufariki kila mwaka kutokana na ugonjwa huu kulingana na takwimu za Shirika la Afya duniani. Malaria, kipindupindu na magonjwa ya kuharisha yanatia shaka mjini Luanda na kwenye miji mingine kutokana na ubovu wa mifumo ya afya na ukusanyaji taka, kama maafisa wa afya walivyoripoti kwenye huduma ya taarifa za Afrika nzima.
6. Nyumba za bei nafuu kupatikana kwa ajili ya maskini na watu wenye maisha ya kiwango cha kati ili waweze kuwatunza watoto wao. Angola ni nchi ya tatu kwa ukubwa wa uchumi kusini mwa jangwa za Sahara Afrika, lakini asilimia 70 ya watu wake wanaishi kwa kiwango chini ya dola 2 kila siku, na zaidi ya asilimia 70 ya watu wa mji mkuu wake wanaishi kwenye vibanda.
7. Wanachama wa kikundi cha maombi cha Project Hannah nchini wanaowatembelea na kuwatia moyo vipofu, watu wasiokuwa na makazi na walio gerezani. Omba ili walio wengi waitikie kwa upendo wa Mungu na zawadi yake ya wokovu kupitia kwa Yesu Kristo.
8. Hekima kwa viongozi wa Angola katika juhudi zao za kugawanya uchumi na kuingia kwenye kilimo, uvuvi na uchimbaji wa madini ili uchumi wa Angola uimarike baada ya kuporomoka kwa kiwanda cha mafuta kwa kiwango kikubwa. Uchumi wa Angola umekuwa ukitegemea mafuta kwa kiwango kikubwa, ukidai kuwa asilimia 95 ya mapato ya vitu wanavyouza nje ya nchi na zaidi ya theluthi mbili ya ushuru wa serikali. Kugawanyika huku kwa uchumi kunaweza kusawadia maelfu ya watu wa Angola kuepuka umaskini.
9. Wanawake wa Angola wapate fursa ya kusikia vipindi vya *Wanawake wa Matumaini*. Taarifa za BBC zinasema serikali inamiliki uchumi na vyombo vyote vya habari kote vinakosikika, ikiwa ni pamoja na redio, kifaa chenye mguso mkubwa nje ya mji. Angola ilikuwa na watumiaji wa mtandao milioni 4.2 kufikia mwaka 2014. *(Internetlivestats.com)*.
10. Angola kuruhusu vipindi vya *Wanawake wa Matumaini* vya kireno kurushwa mahospitalini.
11. Wanawake walio gerezani kufahamu kuwa Mungu hajawaacha na kwamba anaweza kuwapa maisha mapya yenye kusudi. Waombee wanawake wanaohudhuria vipindi vya mafundisho ya uanafunzi kila mwezi kwenye gereza la Luanda huko Angola.
12. Ugawaji wa redio zinazotumia mionzi ya jua zinazofanya walio wengi kusikiliza vipindi vya *Wanawake wa Matumaini*. Mtukuze Mungu kwa ajili ya wafadhili wanaozitoa redio hizi za kipekee.
13. Wasichana wafahamu kuwa wanathaminiwa na Mungu na kwamba ana kusudi kwa ajili ya maisha yao. Omba ili watiwe moyo kupata elimu ya kujilinda kutokana na ndoa za watoto, uzinzi na unyanyaswaji.
14. Wanawake wasiojua kusoma wanaopokea taarifa za thamani kutoka kwenye vipindi vya *Wanawake wa Matumaini*. Mtukuze Mungu kwa ajili ya wanawake wa kushangaza kwenye vikundi vya maombi nchini Angola na Msumbiji wenye mahitaji ya maombi ya Project Hannah yanayotafsiriwa kwa lugha zao kwa njia ya sauti maana hawawezi kusoma. Kazi yao ya maombi ni muhimu sana kwa kile anachokifanya Mungu barani Afrika na